

Mwanaadamu ana mahitaji ya msingi , japokuwa mazingira yanaweza kumuathiri . yametajwa mahitaji hayo ya msingi katika hadith za mtume zilizo sahihi.

Sunnah	Hukmu	Maelezo
[1] Kupunguza sharubu.	Sunnah na inachukizwa kuzinyoa zote.	Sunnah katika sharubu ni kuzipunguza na kuzihafifisha hadi kudhihiri ncha za midomo.
[2] Kufuga ndevu	Wajibu	Ni haramu kunyoa ndevu kwa sababu n Kwenda kinyume na amri ya mtume ya kuzifuga.
[3] Mswaki	Sunnah iliosisitizwa	Kutumia mti wa “Araak” na mfano wake katika kusafisha meno ni sunna katika kila wakati na inahimizwa zaidi wakati wa udhu na wakati wa swala na wakati wakuvingia nyumbani na msikitini na wakati wa kusoma Qur-an na kuamka kutoka usingizini na kwa aliyefikiwa na umauti na pindi inabobadilika harufu ya mdomo.
[4] Kupandisha maji puani	Katika sunnah za udhu	Kuosha pua kwa njia ya kuingiza maji puani na kuyatoa.
[5] Kukata kucha	Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40.	Kukata kucha kwa sababu kuziacha ni sababu ya kukusanyika uchafu chini yake.
[6] Kuosha pingili za vidole	Sunnah	Kusafisha sehemu ambazo unakusanyika uchafu, nazo ni pingili za vidole.
[7] Kunyofoa nywele za kwapa	Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40	Kuondosha nywele zenye kuota kwapani sawasawa zimeondoshwa kwa kunyofoa au kunyoya au kwa njia nyengine, kwa sababu kuondosha kwake ni usafi na kukata harufu yenye kuchukiza.
[8] Kunyoya kinena	Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40	Nywele zenye kuota sehemu za siri. Zinaweza kutolewa pasi na kuzinyoa, kama kutumia mafuta ya kisasa.
[9] Kustanji	Katika adabu za kukidhi haja.	Kuondosha vinavyotoka katika njia mbili kwa kuosha kwa maji na mfano wake katika sehemu inayotoka na zilizo karibu.
[10] Kusukutua	Katika sunna za udhu	Kuosha mdomo kwa njia ya kuingiza maji kisha kuyatoa.
Kutoka kwa Aisha Allah amridhie amesema :Amesema mtume (ﷺ) : Mambo kumi ni katika fitrah: Kupunguza sharubu, Kufuga ndevu, kupiga mswaki, Kupandisha maji puani, kukata kucha, Kuosha pingili za vidole, kunyofoa nywele za kwapa, kunyoya kinena na kustanji. Amesema Zakariyya: Amesema Mus-ab nimesahau jambo la kumi , lakini inaweza kuwa kuskutua. (Imesimuliwa na muslim)		
[11] kutahiri	Wajibu tkwa wanaume sunna kwa wanawake	Kukata ngozi inayofunika dhakar; ili usikusanyike uchafu ndani yake, na ili kutakasika na mkojo.
Kutoka kwa Abu hurayra Allah amrdhie kutoka kwa mtume (ﷺ), amesema: “Mambo matano ni katika fitra: Kutahiri...” imesimuliwa na (Bukhari and Muslim)		